**OMBI LA WOKOVU**
Unaweza kuomba ombi hili kutoka moyoni ombi lako kwa uaminifu kwasababu anakupenda.

Mpendwa Bwana Yesu.

Asante kunisaidia wakati sikuweza kujisaidia. Ninaungama kwako kwamba nimetenda dhambi na kufanya vitu kinyume na mapenzi yako. Tafadhali nisamehe na unitakase kutoka kwa dhambi zangu zote. Tafadhali njoo moyoni mwangu na unibadilishe ili niweze kukutumikia kwa ukweli maishani mwangu. Natambua pasipo wewe, sinatumaini ulimwenguni lakini nikiwa na wewe ninao uzima wa milele. Bwana Yesu ninakushukuru. Sasa mimi ni wako na ninafurahi ndani yako kama mwokozi wangu na naweza kukuita bwana sasa kwa ukweli.
Amina.
kama unajua unamwitaji Bwana Yesu awe mwokozi. Atajibu



Kasisi Patrick na
mke wake Alice


**Anuani yake**
**Missionary Fellowship of Kenya**
**PO Box 145 Bungoma, Kenya**

**Contact Rev Patrick Okumu**
**0727776232**
**Email patweke@yahoo.com**



**Tract produced by revivalUk**
**www.revivalUK.org.uk**
**contact@revivaluk.org.uk**


**Missionary Fellowship of Kenya**

# WOKOVU KAMILI -

# JAMBO AMBALO YESU KRISTO AMEKUFANYIA



www.revivalUK.org.uk

## WOKOVU KAMILI -

## JAMBO AMBALO YESU KRISTO AMEKUFANYIA

Katika Biblia kwa kitabu cha waraka kwa Warumi 5:7 inasema kwamba wakati hatuna nguvu za kujisaidia wenyewe Kristo alikufa kwa ajili ya wasiomjua Mungu, na tena msitari wa 8 unasema kwamba Mungu ametuonyesha upendo wake kwamba wakati tungali wenye dhambi yesu alitufia sisi.

Hii misitari miwili au 2 inanena juu yetu na tena inanena kumhusu Bwana Yesu, inatuambia ya kwamba hatuna uwezo wa kujiokoa wenyewe, na kitu kinachotusumbua ni dhambi zetu, kwa mfano mtu akitaka kujiokoa katika hatari ya kuzama ndani ya mto wa kilindi kirefu na kama hangeweza kufanya hivyo lazima msaada upatikane na mwingine aje amuokoe, kama watu wangeweza kujiokoa wenyewe wasingetaka wasaidiwe.

Huu ni mfano wa kweli kuhusu wokovu wetu, tunahitaji kuokolewa katika hali ile tunayo, hakuna kitu kitakachoweza kufanya tujiokoe wenyewe, katika waraka kwa Warumi 3:23 inasema kwa sababu wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu, na kwa hivyo kila mtu anahitaji kuokolewa, shida yetu kuu ni dhambi.

Mtu wa kwanza Adam alitenda dhambi na sasa dhambi ikaingia katika asili ya mwanadamu na hivyo ikaendelea kuwa katika kila kizazi, unaweza kuona matunda ya dhambi katika jamii ya watu kwa wengine, kwa mfano kuna tabia kama kuiba, chuki, uasherati na mengine mengi ikitendeka, hiyo ndiyo kazi inayotendeka kwa sababu ya asili ya dhambi zinazokaa ndani ya watu, jambo ni kwamba hatuamini neno la Mungu na kazi aliyotutendea, tamaduni nyingi katika ulimwengu zimeachana na neno la Mungu, na watu wanaishi tu maisha isiyo na wokovu wa Yesu Kristo.

Hakuna mwanadamu yeyote ameishi kiwango cha haki ambayo Mungu anataka, kwa hivyo kwa asili zetu sisi ni wana wa ghadhabu na tuna haja kubwa ya kupokea wokovu.

Lakini Mungu anatupenda na anaweza kutufanyia njia ya kuepuka na dhambi ili tupate msamaha wa dhambi zetu na haki katika kumkiri Mwanawe Yesu Kristo, Mungu ametimiza hayo wakati ambapo tunahitaji sana kumkaribia wakati tumekuwa katika upotevu na katika dhambi.

Hatuwezi kujirekebisha sisi wenyewe katika maisha yetu, lakini Yesu alitufia tulipokuwa tungali wenye dhambi, jibu ametupa tayari.

Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, jiulize mbona afe? Ilikuwa ni bora mmoja achukue hukumu ya Mungu kwa ajili ya dhambi zetu, ilikuwa ni hukumu ya kweli kwamba Yesu atufie sisi, alimwaga damu yake kwa ajili ya maisha yetu yote, akafufuka tena kutoka ndani ya wafu, ilidhihirisha ya kwamba alishinda dhambi na mauti, kuonyesha kwamba wokovu wake ndio njia ya pekee ya kweli, Yesu ametukomboa katika damu yake mwenyewe kwa kulipa gharama ya dhambi zetu ili sisi tufanyike wana wa Mungu.

Swali ni hii, tutapataje wokovu huu? Lazima kuungama ahadi zake kwetu, tunaacha njia zetu mbovu na kutubu kabisa dhambi zetu kwa Mungu na yeye ni mwaminifu kwa kuweza kutusamehe kabisa na kutusafisha kutokana na kila uovu wote tumetenda katika mioyo yetu.

